
# HUDUMA YA KWANZA KATIKA KUTIBU JERAHA ZA KUUNGUA



## Kijitabu kwa ajili ya Wahudumu wa Afya Wafanyao Kazi kwenye Ngazi ya Jamii

Interburns

ONGEZA NEMBO YAKO HAPA

# UTANGULIZI JUU YA JERAHA ZA KUUNGUA

## JERAHA ZA KUUNGUA NI NINI?

Jeraha la Kuungua ni jeraha lililopo kwenye ngozi ya mtu kwa kawaida likiwa limesababishwa na moto, kimiminika, umeme au kemikali. Majeraha yaliyoungua yanaweza kutofautiana kati ya yale **madogo yanayoweza kutibiwa nyumbani**, na yale majeraha ma**kubwa sana yanayohitaji matibabu ya dharura** hospitalini, na majeraha hayo yanaweza hata kusababisha kifo katika baadhi ya hali mahututi.

**Kama mhudumu wa afya wa jamii**, ni muhimu kua na ujuzi wa kuweza kutofautisha kati ya jeraha dogo na kubwa la kuungua. Kisha utaweza kujua wakati gani jeraha la kuungua linaweza kutibiwa katika kituo chako cha afya, au wakati gani hali huwa mbaya zaidi na kuhitaji kupelekwa hospitalini.

Katika muongozo huu, tumeangazia baadhi ya ishara muhimu zaidi za kuzitazama pale unapoletewa mgonjwa mwenye jeraha la kuungua, ili uweze kupanga matibabu sahihi, na kujua kama mgonjwa huyo atapaswa kwenda hospitalini au la.



Jambo la kwanza unalopaswa kutathmini kwa mgonjwa mwenye jeraha la kuungua ni **wapi** anapaswa kutibiwa.

- Je, anaweza kutibiwa nyumbani?
- Je, anaweza kutibiwa kwenye kituo cha afya?
- Je, anapaswa kupelekwa kwenye kituo kikubwa zaidi cha afya kwa ajili ya matibabu?



Kuna mambo mengi yatakayokusaidia kujibu maswali haya, hata hivyo baadhi ya mambo muhimu zaidi ni:

➔ Ukubwa wa jeraha la kuungua
➔ Aina ya jeraha la kuungua
➔ Eneo la mwili lililoathiriwa na jeraha la kuungua

**Kijitabu hiki kitasaidia kueleza kwa namna gani tofauti zilizopo katika mambo haya huathiri mpango wa matibabu ya mgonjwa.**

## AINA ZA JERAHA ZA KUUNGUA

Kuna visababishi vikuu vitano vya jeraha za kuungua:



**Majeraha ya kuunguzwa na moto:** Haya hujumuisha majeraha yaliyosababishwa na moto, mfano kutoka kwenye kuni, majiko ya mkaa, majiko ya mafuta ya taa, jeraha zilizosababishwa na baruti za sherehe na ajali za moto nyumbani.



**Majeraha ya kuunguzwa na michemko:** Haya hujumuisha majeraha yaliyosababishwa na vimiminika vya moto, mfano kutoka kwenye maji yanayochemka, chai, kahawa, maziwa,supu n.k.



**Majeraha ya kuunguzwa na sehemu za moto:** Haya hujumuisha majeraha yaliyosababishwa na kugusa vitu vya moto mfano chombo cha moto cha jikoni au pasi.



**Majeraha ya kuunguzwa na umeme:** Haya hujumuisha majeraha yaliyosababishwa na umeme mfano nyaya za umeme wa volteji kubwa, tundu za umeme na umeme wa radi.



**Majeraha ya kuunguzwa na kemikali:** Haya000 hutokana na kumwagikiwa kemikali kwenye ngozi. Mfano madawa ya kusafisha chooni nyumbani, viuwa vijidudu, na kemikali za betri, mashambulio ya tindikali huhesabika pia kama majeraha ya kuunguzwa na kemikali.

## NAMNA YA KUFAHAMU WAKATI WA KUMKATIA MGONJWA RUFAA

**'Kupata rufaa' humaanisha kumhamisha mgonjwa kwenda hospitali kubwa zaidi, hasa ile iliyobobea katika matibabu ya majeraha ya moto, kwani mahitaji yake hayawezi kukidhiwa katika kituo kidogo husika cha afya.*

Kama jeraha ni kubwa, basi mgonjwa atapaswa kukatiwa rufaa.

**Unajuaje kama jeraha ni kubwa?**

Kumbuka

a) kadri mtu alivyowekwa kwenye chanzo cha moto kwa *muda mrefu zaidi*, ndivyo kadri jeraha litakavyokuwa katika hali mbaya zaidi, na

b) kadri eneo/kimiminika/moto uliogusa ngozi husika ulivyokuwa *mkali zaidi*, ndivyo kadri jeraha litakavyokuwa katika hali mbaya zaidi.

Ingawa ni ngumu kujua uzito wa jeraha hilo, kuna mambo machache unaweza kutazama ili kukusaidia kuamua:

- **Jeraha dogo la kuungua** kwa kawaida litatengeneza eneo la wekundu kwenye ngozi iliyojeruhiwa, na awali litaonekana kuloa. Aina hii ya jeraha mara nyingi huwa na maumivu makali sana. Kama jeraha hili limeathiri sehemu ndogo tu ya mwili, mfano sehemu ya mkono, litaweza kutibiwa kwenye kituo cha afya au nyumbani. Kama aina hii ya jeraha limefunika sehemu kubwa ya mwili, mfano mkono mzima, sehemu kubwa ya mkono, mguu au uso, mgonjwa atabidi kukatiwa rufaa kwenda hospitali kubwa zaidi.

- **Jeraha kubwa zaidi la kuungua** litaonekana kuwa kavu, na linaweza kuwa na malengelenge na uvimbe. Jeraha hili, ingawa ni kubwa zaidi, huwa na maumivu kidogo zaidi kwa mgonjwa. Wagojwa wengi wenye aina hii ya jeraha watahitaji kukatiwa rufaa kwenda hospitali kubwa zaidi. Wale tu walioathirika sehemu ndogo ya mwili, kwa mfano wa ukubwa wa sarafu, ndio wanapaswa kutibiwa kwenye kituo cha afya

- **Aina mbaya zaidi ya jeraha la kuungua** litaonekana kuchomeka au leupe. Majeraha haya yanakuwa magumu ukigusa, pia hakutakuwa na hisia yoyote ya maumivu kwenye eneo la jeraha. Aina hii ya jeraha sharti ikatiwe rufaa ya kwenda hospitalini haraka.

**Mambo mengine ya kukusaidia kuamua kama unapaswa kumkatia mgonjwa rufaa**

Kumbuka, majeraha mengi ya kuungua yanaweza kutibiwa kwenye kituo cha afya, na majeraha makubwa mengi ya kuungua yanaapaswa kukatiwa rufaa kwenda hospitali kubwa zaidi.

Hapa ni mambo  machache zaidi ya kukusaidia kuamua kama mgonjwa wako anahitaji kukatiwa rufaa au la.

- Kama jeraha dogo liko kwenye eneo nyeti, ni bora zaidi kumkatia mgonjwa rufaa, hata kama ukiwa hauna uhakika kama jeraha hilo ni kubwa kutosha kukata rufaa, kwani maeneo haya yanaweza kusababisha ugumu zaidi katika matibabu.



  - **‘Eneo nyeti’ ni zipi?**: kichwa, shingo, viungo, mikono, uso, tumbo na sehemu za siri.




- Kama mgonjwa ana umri mdogo sana au ni mzee sana, ni bora ukamkatia rufaa isipokuwa kama jeraha lake ni dogo sana.



- Kama mgonjwa hana familia, inaweza kuwa vema zaidi kumkatia rufaa ili kuhakikisha anapata uangalizi wote anaouhitaji

- Kama jeraha ni dogo lakini liko sehemu kubwa ya mwili, zingatia kumkatia rufaa.
  - **Sehemu ‘kubwa’ ya mwili ni kiasi gani?**: Kwa mfano, mkono wote, eneo kubwa la mgongo na/au kifua, sehemu kubwa ya mkono, sehemu kubwa ya mguu.



- Kama mgonjwa ameunguza uso wake, ama ana dalili yoyote ya kuwa na jeraha katika upumuaji (jeraha katika njia za hewa au mapafu), atahitaji kukatiwa rufaa.
  - **Ni zipi baadhi ya dalili za jeraha katika upumuaji?:** Kukohoa au makohozi, koo linalokwaruza, ugumu wa kupumua, maumivu ya kifua au kubanwa kifua, maumivu ya kichwa, macho kuwasha.



- Daima kata rufaa kama jeraha ni la kuunguzwa na kemikali au umeme - bila kujali ukubwa wa jeraha hilo.

- Kama jeraha halionyeshi kupona ndani ya siku chache za kwanza  au linaonekana kama limepata maambukizi, mgonjwa atabidi kukatiwa rufaa.

Kama mgonjwa yuko katika hali mahtuti na anahitaji usaidizi wa dharula wa kuokoa maisha yake, atapaswa kukatiwa rufaa kwenda hospitali ya karibu.

## MWITIKIO WA AWALI NA HUDUMA YA KWANZA

Kama upo kwenye eneo la mjeruhiwa, kwanza **ondoa chanzo cha jeraha hilo la kuungua** mfano: zima moto, ondoa kifaa cha moto kilichopo. Kama mtu anawaka moto, anapaswa kushauriwa “***kusimama, kulala chini na kujiviringisha***” ili kuzima moto huo.



Kisha **huduma ya kwanza** inapaswa kufanyika. Hakikisha kwamba ucheleweshwaji ni mdogo katika kutoa huduma ya kwanza kwani hili humsaidia mgonjwa kupata nafuu, kupunguza hatari ya matatizo na huweza pia kupunguza uwezekano wa makovu na maambukizi baadae.

Katika kipindi chote cha matibabu, unapaswa kujaribu **kubaki umetulia na kumtia moyo kadri iwezekanavyo** ili kumsaidia mgonjwa kutulia.

**<u>Hatua za Huduma ya Kwanza:</u>**

- Kwenye eneo la jeraha la kuungua kwa moto/joto, *maji masafi* yanapaswa kutiririshwa kwa takribani **dakika 20** kusaidia jeraha hilo lipoe.



- Kwenye jeraha la kuungua kwa kemikali, ni muhimu kusafisha jeraha hilo kwa maji ya kumiminika ili **kuondoa/kuyeyusha kemikali hizo.** Hakikisha kwamba maji hayo yanadondoka *kutoka* kwenye mwili, ili muwasho zaidi usisababishwe: mfano. Kama kemikali iko kichwani, hakikisha maji hayaingii machoni ambapo yanaweza kusababisha madhara zaidi.

  **Kama hamna haja ya kumkatia mgonjwa rufaa, na jeraha hilo la kuungua linaweza kutibiwa kwenye kituo cha afya, basi kufuata hatua zifuatazo kutakusaidia kumpatia mgonjwa huyo matibabu bora:**

- Safisha jeraha kwa sabuni na maji masafi.

- Valisha vazi lenye **tabaka mbili**. Tabaka la kwanza linapaswa lisiwe linalokwaruza, kama vile **vazi la shashi ya vaselini**, kwani hili litasaidia kuweka unyevunyevu kwenye jeraha na kuzuia vazi hilo kunata kwenye ngozi. Tabaka la pili linapaswa kuwa **vazi zito lililotengenezwa na nguo inayofyonza maji** ili kusaidia kufyonza majimaji yoyote yanayotoka kwenye jeraha.

- Vazi jipya linahitajika kuvalishwa mathalani **kila baada ya siku 3-4**, au pale vazi lililopo linapolowa. Hatahivyo, jeraha lililopata maambukizi linahitaji mabadilisho ya vazi kila siku. **Dalili za maambukizi** ni: Kama jeraha litazidi kuwa na maumivu, litaanza kunuka vibaya, au usaa kuanza kutoka kwenye eneo la jeraha. Mgonjwa atapaswa kukatiwa rufaa kama jeraha litapata maambukizi, kwani anaweza akahitaji kupatiwa dawa kutoka hospitalini.

## TAARIFA YA ZIADA KUHUSIANA NA HUDUMA YA KWANZA NA UFUNIKAJI WA JERAHA LA KUUNGUA

Katika baadhi ya jamii, vitu kama kinyesi cha ng’ombe, dawa ya mswaki, mchanga n.k. hutumika kupaka kwenye vidonda vya kuungua. Ni muhimu **kutofanya** haya kwani yanaweza kusabisha maambukizi kwenye kidonda hicho, na kusababisha ugumu katika kupona kwake.

Hakikisha unasafisha mikono yako vizuri na mara kwa mara kabla ya kumgusa mgonjwa. Hili litasaidia kuzuia usambazaji wa vijidudu, na kupunguza uwezekano wa maambukizi.

Pendekeza dawa za maumivu kama vile paracetamol ili kumsaidia mgonjwa kustahimili maumivu yoyote anayoyahisi. Kutulia na kuwahakikishia unafuu kunaweza kuwasaidia kustahimili taabu yoyote ya kisaikolojia wanayoweza kuwa nayo.

Mwekee maji masafi (hupendekezwa ya kumiminika) kwa **dakika 20** ili kupooza kidonda hicho. Baada ya kufanya hivi, kwa umakini ondoa vito vyovyote kutoka kwenye eneo la jeraha, na valisha jeraha hilo vazi safi la tabaka mbili.

Takasa kifaa na chumba cha kusafishia jeraha.

Kama jeraha hilo la kuungua lipo kwenye mikono au miguu, hakikisha unavisha vidole vya mikono/miguu kwa kuvitenganisha.



Wakati wa kutibu watoto, inaweza kusaidia sana kama utatumia midoli au michezo kuwasahaulisha watoto maumivu yoyote yatokeayo wakati wa kutibiwa. Pia, kuwa na wazazi ndani ya chumba hicho kunaweza kusaidia sana.



Kama jeraha halijaonyesha kabisa kupona baada ya wiki 2, mgonjwa huyo atapaswa kukatiwa rufaa kwenda kituo kikubwa zaidi cha afya.



Mgonjwa akishafanyiwa matibabu ya jeraha la awali, **unawezaje kumpatia uangalizi bora katika kipindi cha wiki zinazofuata?**

Hakikisha **unamjumuisha mgonjwa na familia yake** wakati unapopanga na kutoa matibabu ili waelewe na kusaidiana kikamilifu, na kuhakikisha matokeo mazuri ya matibabu.

Katika wiki chache za kwanza, unapomtibu mgonjwa kwenye kituo cha afya, ni muhimu kumfuatilia mgonjwa kuona kama kuna **dalili zozote za maambukizi.** Kama unashuku kuwa jeraha limeambukizwa, utapaswa kumkatia rufaa mgonjwa huyo haraka iwezekanavyo.

**Namna ya kugundua maambukizi:**

Ongezeko la joto

Ongezeko la mapigo ya moyo, hata akiwa amepumzika

Usaa katika eneo la jeraha



### Hakikisha lishe bora

Katika upande wa lishe, ni muhimu kwamba baada ya kupata jeraha hilo, mgonjwa ale lishe bora na kamili inapowezekana, kwani kukosa lishe kunaweza kuchelewesha uponyaji wa jeraha hilo. Pia, jeraha za kuungua zinaweza kumsababisha mgonjwa kupungukiwa maji, hivyo unapaswa kumhimiza mgonjwa kunywa vimiminika, hasa Vinywaji vya Kuchanganya Maji, Sukari na Chumvi kama vitapatikana. Baadhi ya wagonjwa wanaweza kuhitaji kutundikiwa dripu, kama utakuwa na nyenzo hiyo.

### Makovu

Mgonjwa anapokuwa na jeraha kubwa linalochukua zaidi ya wiki tatu kupona, uwezekano wa kovu kutokea ni mkubwa. Katika majeraha makubwa, makovu yanaweza kushamiri na kukomaa. Ni muhimu kwamba familia, marafiki na jamii imsaidie mgonjwa huyo kukubaliana na kujiona na kujihisi tofauti baada ya jeraha kubwa la kuungua. Wanaweza kuonekana kimya na wenye mawazo, hasa kama kovu lao linaonekana au kuungua kwao kumewasababishia kiwango fulani cha ulemavu. Uangalizi mzuri na mtazamo wa kujali kutoka kwa familia na marafiki unaweza kuleta tofauti kubwa katika kumsaidia mgonjwa kwenye huzuni ya kisaikolojia inayoweza kusababishwa na jeraha hilo la kuungua.

